



Usajili wa Shule ya Awali ya Lowell Public Schools

USAJILI WA SHULE YA AWALI YA LOWELL PUBLIC SCHOOLS UTAANZA KUTOKA MACHI 8, 2021: Ili kufanya usajili uwe wenyewe usalama na wepesi zaid iwezekanavyo, usajili sasa unafanyika kupitia mtandao. Tafadhali soma taarifa iliyo kwenye ukurasa huu ili kufahamu mchakato wa usajili. Tarehe ya mwisho kabisa ili kustahiki bahati nasibu ya shule ya awali ni Machi 28, 2021 saa 11:59 jioni. Tafadhali hakikisha umewasilisha usajili wako kabla ya tarehe hii. Baada ya tarehe hii ya mwisho, wanafunzi watakaojisajili kwa shule ya awali wataongezwa katika orodha ya wanaongojea na hawataongezwa katika bahati nasibu.

Mikutano ya Mbali ya Taarifa Kuhusu Shule ya Awali

Jifunze zaidi kuhusu programu yetu ya shule ya awali na mchakato wa usajili katika mojawapo wa mikutano zetu za usiku za kuarifiwa kwa mbali! Mikutano katika Kiingereza, Kihispania, Kireno, Ki-Khmer & Kiswahili.

- Jumanne, Machi 2 mnamo 6:30 jioni kupitia Zoom

Kiswahili (Swahili):

<https://lowell-k12-ma-us.zoom.us/j/4113779530>

Kiingereza (English):

https://lowell-k12-ma-us.zoom.us/webinar/register/WN_Fr0yYihJQoWNfa5ZWVewkA

- Alhamisi, Machi 4 mnamo 12 jioni kupitia Zoom

Kiswahili (Swahili):

<https://lowell-k12-ma-us.zoom.us/j/4113779530>

Kiingereza (English):

https://lowell-k12-ma-us.zoom.us/webinar/register/WN_gqvmONPMQjyZKqZ330NYhg

Katika programu yetu ya shule ya awali, mtoto wako atakuza ujuzi wa kijamii, kilugha, kuandika na kusoma, hesabu na sayansi zinazohitajika katika shule ya kimsingi na mbele zaidi! Ili

kujifunza zaidi kuhusu programu zetu za shule ya awali tafadhali tembelea our [tovuti letu la Utoto wa Mapema](#).

Ni nani Anafaa Kujisajili katika Shule ya Awali?

Watoto wanaoingia mwaka wao wa 4 kufikia au kabla ya Septemba 1, 2021 wanastahiki kujisajili kwa shule ya awali. Watoto wanaopokea huduma za Elimu Maalum wanastahiki kujisajili katika shule ya awali wakitimiza umri wa miaka 3.

Kabla Hujajisajili:

- Tambua chaguo tatu za shule. Unaweza kuchagua shule zozote tatu zinazotoa programu za shule ya awali. Tafadhali rejelea [cheti hii](#) kwa orodha ya shule zinazoweza kupatikana zilizo na nafasi ya shule ya awali.
- Kadiri wakati wa kuanza na kuisha kwa kila shule, pamoja na mahitaji yako ya utunzaji mtoto kabla ya na baada ya shule. Tafadhali kumbuka kwamba huduma ya usafirishaji kwa wanafunzi wa shule ya awali HAITOLEWI na wilaya. Mafamilia wana wajibu wa kusafirisha watoto.
- Kusanya hati zinazohitajika katika usajili zikiwamo:
 - Cheti cha kuzaliwa cha mtoto
 - Rekodi za chanjo za mtoto
 - Hati ya Utambulisho iliyo na picha ya mzazi/mlezi anayesajili mtoto
 - Ushahidi wa ukaazi (nakala ya risiti ya gharama ya matumizi ya sasa, ya kukodisha, au mkopo wa rehani ambayo tarehe yake imo katika siku za thelathini zilizopita)
 - Iwapo unaishi na mkaazi wa Lowell, utahitaji kukamilisha hati ya kiapo. Tafadhali zungumza nasi iwapo huwezi kutoa ushahidi wa kutosha au iwapo nyumba yako haina usalama. Tunafuata sheria ya McKinney-Vento. Tafadhali fuata kiungo au link ifuatayo kwa [Taarifa zaidi kuhusu hati za kiapo na sheria ya McKinney-Vento](#).

Mchakato wa Usajili:

- Sajili mtoto wako kwenye mtandao kati ya Machi 8, 2021 na Machi 28, 2021 kabla ya saa 11:59 jioni ili kuweza kushiriki katika bahati nasibu. Usajili unafanywa kati ya Jumatatu hadi Ijumaa 8:00 asubuhi hadi 4:00 jioni, lakini usajili unaweza kuwasilishwa kwenye mtandao wakati wowote.

- **Link au kiungo kwa fomu ya Usajili utaweza kupatikana kutoka Machi 8, 2021.**
- Pindi unapowasilisha fomu ya usajili, utaweza kupokea barua pepe kutoka Kituo cha Rasilimali ya Kitaarifa kwa Familia inayokuomba kuambatanisha hati za ushahidi kama:
 - Cheti cha kuzaliwa cha mtoto na Rekodi za chanjo za mtoto
 - Hati ya Utambulisho iliyo na picha ya mzazi/mlezi anayesajili mtoto
 - nakala ya risiti ya gharama ya matumizi ya sasa, ya kukodisha, au mkopo wa rehani
- Pindi unapowasilisha hati zote zinazohitajika utapokea barua pepe ya kufuatilia kutoka karani uliyopewa akikuarifu kuhusu hali ya usajili wako.

Bahati Nasibu ya Shule ya awali

- Bahati nasibu ya Shule ya awali itatendeka kufikia Mei 31, 2021. Tutawaarifu kuhusu tarehe pindi itakapoamuliwa.
- Watoto wote wanaofanya usajili wa awali watapatiwa nambari ya bahati nasibu.
- Mafamilia ambazo zimefanya usajili hapo awali zitapokea arifa inayopea nambari ya bahati nasibu ya mwanafunzi na shule anayependekeza kuteuliwa.
- Baada ya kupokea arifa ya barua kutoka shule ya awali iliyoteuliwa, NI LAZIMA familia wajibu huku wakichagua mojawapo ya yafuatayo:
 - Kukubali mpangilio
 - Kukubali mpangilio na kubaki katika orodha ya wanaoongoja ili kuongoja shule unayopendelea
 - Kukataa mpangilio na kubaki katika orodha ya wanaoongoja ili kuongoja shule unayopendelea
 - Kukataa mpangilio na kutafuta mpango mwingine wa shule ya awali

NI LAZIMA familia warejeshe barua ya uteuzi wa shule uliopendekezwa ndani ya siku 15 kwa Idara ya Utoto wa Awali ikionyesha mojawapo ya chaguo zilizo hapa juu.

Uteuzi kwa Shule ya awali

- Baada ya kupokea barua yako ya chaguo lako, Idara ya Utoto wa Awali watatoa barua rasmi ya uteuzi kwa shule.

- Iwapo una swali kuhusu mpangilio wa mtoto wako, unaweza kuwasiliana na:
 - Lisa Van Thiel, **Simu:** 978-674-2051 **Barua Pepe:** ivanthiel@lowell.k12.ma.us
 - Susan LaCroix, **Simu:** 978-674-2050 **Barua Pepe:** slcroix@lowell.k12.ma.us
 - Laurie Carney, **Simu:** 978-446-7000 Ext.
46919 **Barua Pepe:** lauriecarney@lowell.k12.ma.us
- Kufikia mwezi wa Agosti utapokea arifa kutoka kwa shule ya mtoto wako ikiwa na mpangilio wa mwalimu wao.

Taarifa ya Mawasiliano ya Karani wa Usajili wa FRC

- Lynn Moran - **Simu:** 978-674-2074 **Barua Pepe:** lmoran@lowell.k12.ma.us
- Pat Noonan - **Simu:** 978-674-2071 **Barua Pepe:** pnoonan@lowell.k12.ma.us
- Vaddy Ros - **Simu:** 978-674-2073 **Barua Pepe:** vros@lowell.k12.ma.us (anaweza kuzungumza katika lugha ya Ki-Khmer)
- Elsa Sanchez - **Simu:** 978-674-2072 **Barua Pepe:** esanchez@lowell.k12.ma.us (anaweza kuzungumza katika lugha ya Kihispania)